

**MWONGOZO WA KUANDAA MPANGO NA BAJETI YA  
SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/17**

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO,

**FEBRUARI, 2016**



## **YALIYOMO**

1.0	UTANGULIZI .....	1
2.0	MAPITIO YA UCHUMI NA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI .....	2
3.0	MABORESHO YA MFUMO WA BAJETI.....	7
3.1	Sheria ya Bajeti .....	7
4.0	MAANDALIZI YA MIPANGO NA BAJETI ZA TAASISI.....	7
4.1	Kamati za Bajeti.....	7
4.2	Ratiba ya Maandalizi ya Mpango na Bajeti .....	8
4.3	Mchakato wa Uchambuzi wa Bajeti .....	8
4.4	Uingizaji wa Takwimu za Bajeti Katika Mfumo wa Malipo .....	9
5.0	MAELEKEZO YA MAANDALIZI YA BAJETI.....	9
5.1	Mfumo wa Mapato na Matumizi Katika Kipindi cha Muda wa Kati .....	9
5.2	Viwango vya Ukomo wa Bajeti Katika Kipindi cha Muda wa Kati .....	10
5.3	Mikakati ya Kuongeza Mapato.....	10
5.4	Vigezo vya Kugawa Rasilimali .....	11
6.0	MAMBO MENGINE YA KUZINGATIWA KATIKA UANDAAJI WA BAJETI .....	15
6.1	Kudhibiti Ulimbikizaji wa Madeni .....	15
6.2	Madeni yatokanayo na dhamana za Serikali kwa Mashirika .....	15
6.3	Hatua za kudhibiti matumizi .....	16
6.4	Kiwango cha kubadilisha fedha .....	17
6.5	Kujumuisha Masuala Mtambuka Katika Mpango na Bajeti .....	17
6.6	Utawala Bora na Utawala wa Sheria.....	17
6.7	Ajira na Uwezesaji wa Kiuchumi .....	18
6.8	Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa .....	18
6.9	Usimamizi wa Mali za Umma.....	19
6.10	Ushirikiano kati ya Sekta ya Umma na Binafsi .....	19
7.0	MAELEKEZO MAHSUSI KWA SEKRETARIETI ZA MIKOA NA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA .....	20
8.0	UFUATILIAJI, TATHIMINI NA UTOAJI TAARIFA .....	22
8.1	Utoaji wa Taarifa za Utendaji.....	22
8.2	Mwisho .....	23



# **MWONGOZO WA KUTAYARISHA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2016/17**

## **1.0 UTANGULIZI**

1. Mwongozo wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2016/17 umeandaliwa kwa kuzingatia Kifungu Na. 21 cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya Mwaka 2015. Aidha, Mwongozo wa Mpango na Bajeti wa Mwaka 2016/17 umejikita katika kujenga Taifa lenye uchumi wa viwanda kama ilivyoainishwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2016/17 pamoja na Mpango Elekezi wa Miaka 15. Vile vile Mwongozo huu unajielekeza katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015, Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025.

2. Katika kuhakikisha kunakuwa na maendeleo ya haraka na endelevu ya viwanda, Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2016/17 utalenga kutumia kikamilifu fursa na rasilimali za nchi zikijumuisha kilimo, jiografia ya nchi, utalii, nguvu kazi ya kutosha (katika viwanda), masoko ya ndani na ya kikanda, na upatikanaji wa rasilimali asili. Hivyo, kipaumbele katika kujenga msingi wa nchi ya viwanda kitazingatia: uendelezaji wa viwanda vinavyotumia malighafi za hapa nchini (viwanda vya kusindika malighafi za kilimo, pembejeo za kilimo, viwanda vya nguo, ngozi, madawa, viwanda vya kati na viwanda vya kuchakata madini); Viwanda vinavyotumia fursa ya kijiografia ya nchi yetu; Viwanda vinavyoajiri watu wengi; viwanda vinavyokidhi mahitaji ya mijini; viwanda vya sayansi, teknolojia na ugunduzi na vya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano; na maendeleo ya rasilimali watu. Ili kuhakikisha kunakuwa na mazingira wezeshi ya maendeleo ya viwanda, vipaumbele vitakavyozingatwa ni pamoja na: kuboresha mazingira ya biashara; na utekelezaji wa miradi inayoendelea ya Mpango wa kwanza wa maendeleo hususan miradi ya miundombinu ikiwemo umeme wa uhakika na wa gharama nafuu.

3. Ili kuwa na ufanisi na matumizi bora ya rasilimali chache ilizopo, Mwongozo wa Mpango na Bajeti wa mwaka 2016/17 utajielekeza katika kutekeleza Sheria ya Bajeti namba 11 ya mwaka 2015 ili kutoa miongozo kwa maafisa masuuli kuandaa mipango na bajeti kwa ufasaha. Aidha, Mwongozo unasisitiza juu ya umuhimu wa kuzingatia Maelekezo ya uandaaji na usimamizi wa miradi ya uwekezaji wa umma (PIM-OM) kama mwongozo mkuu katika kuandaa miradi ya maendeleo. Hivyo, Wizara, Idara zinazojitegemea, Taasisi na Wakala za Serikali (MDAs), Sekretarieti za Mikoa (RSs), Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs) na taasisi nyingine za umma (ikijumuisha mashirika na mifuko ya hifadhi za jamii) zinaelekezwa kutenga fedha katika maeneo ya kimkakati ambayo yatachochea ukuaji wa viwanda na maendeleo ya watu.

4. Mwongozo wa Mpango na Bajeti umeandaliwa katika sehemu sita, ambazo ni: utangulizi ambao unatengeneza msingi wa Mwongozo wenyewe; Mapitio ya uchumi na utekelezaji wa bajeti ya Serikali; maandalizi ya mipango na bajeti za taasisi; maelekezo ya kuandaa mpango na bajeti; maeneo mengine muhimu ya kuangalia wakati wa kuandaa bajeti; maelekezo mahsusi kwa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; ufuatiliaji, tathmini na uandaaji taarifa; na hitimisho.

## **2.0 MAPITIO YA UCHUMI NA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI**

### **Mwenendo wa Viashiria vya Uchumi**

5. Uchumi wa Taifa umeendelea kuimarika ambapo mwaka 2014 ulikua kwa asilimia 7.0. Aidha, katika kipindi cha Januari hadi Septemba 2015, uchumi umekua kwa wastani wa asilimia 6.9 ikilinganishwa na wastani wa asilimia wa 8.0 katika kipindi kama hicho mwaka 2014 kwa bei za mwaka wa kizio wa 2007. Ukuaji huu umechangiwa kwa kiasi kikubwa na sekta ya ujenzi kutokana na utekelezaji wa miradi mikubwa ya miundombinu ya barabara na nishati na ujenzi wa majengo ya biashara na makazi. Mfumuko wa bei ulipungua kufikia wastani wa asilimia 4.0 Januari, 2015 na kuongezeka kufikia asilimia 6.1 Juni, 2015 ikilinganishwa na lengo la asilimia 5.0 kwa kipindi hicho.

6. Thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma nje iliongezeka kwa asilimia 8.3 kutoka Dola za Kimarekani milioni 8,589.3 mwaka 2013/14 hadi Dola za Kimarekani milioni 9,299.8 mwaka 2014/15. Hata hivyo, thamani ya uagizaji wa bidhaa na huduma mwaka 2014/15 ilipungua kutoka Dola za Kimarekani milioni 13,966.2 mwaka 2013/14 hadi Dola za Kimarekani milioni 13,370.1 sawa na asilimia 4.3 kutokana na kupungua kwa thamani ya uagizaji wa mafuta kwa asilimia 27.2 katika kipindi hicho.

7. Katika kipindi cha mwaka 2014/15 thamani ya shilingi dhidi ya Dola ya Marekani imekuwa na mwenendo usioridhisha. Thamani ya shilingi imepungua kwa asilimia 24.1 kutoka wastani wa shilingi 1,731.31 kwa dola moja mwezi Novemba 2014 hadi shilingi 2,149.1 kwa dola moja mwezi Novemba 2015. Hali hii imetokana na kuimarika kwa uchumi wa Marekani pamoja na kupungua kwa mapato ya mauzo nje ikilinganishwa na mahitaji ya kuagiza huduma na bidhaa kutoka nje. Serikali ilichukua hatua mbalimbali za kuimarisha thamani ya shilingi ikiwa ni pamoja na kuongeza kiwango cha amana kwa benki za biashara wanachotakiwa kuhifadhi Benki Kuu. Aidha, Serikali itahakikisha inapata suluhisho la muda mrefu ambalo ni upatikanaji wa umeme wa uhakika na kuimarisha uzalishaji viwandani ili kuongeza mauzo nje ya bidhaa za viwandani.

## **Utekelezaji wa Bajeti 2014/15**

8. Katika mwaka 2014/15, Serikali ilikadiria kukusanya na kutumia shilingi bilioni 19,853.3. Kati ya kiasi hicho, mapato ya ndani yakijumuisha ya Halmashauri yalikalidiriwa kuwa shilingi bilioni 12,636.5; na misaada na mikopo shilingi bilioni 2,941. Katika mwaka 2014/15, mapato ya ndani yalifikia shilingi bilioni 11,013 sawa na asilimia 89 ya makadirio ya mwaka, ikiwa ni ongezeko la asilimia 6 ikilinganishwa na mapato yaliyokusanywa katika mwaka 2013/14. Mapato ya kodi yalifikia shilingi bilioni 9,938.4 sawa na asilimia 87.8 ya makadirio. Sababu za kutofikia malengo ni pamoja na kushuka kwa shughuli za utafiti na utafutaji wa madini, mafuta na gesi ambazo hutozwa kodi ya zuio; anguko la bei katika soko la dunia hasa kwenye dhahabu; na kushuka kwa bei ya baadhi ya bidhaa kutoka nje hususan mafuta ya petroli.

9. Kwa upande wa matumizi, jumla ya shilingi bilioni 17,189.7 zilitumika, ikiwa ni asilimia 87 ya makadirio ya mwaka 2014/15. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 13,928.0 zilikuwa ni matumizi ya kawaida, sawa na asilimia 4 zaidi ya lengo kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya kugharamia uchaguzi mkuu. Matumizi ya maendeleo yalikuwa shilingi bilioni 3,261.7, sawa na asilimia 51 ya lengo. Upungufu huo ulitokana na kupungua kwa misaada na mikopo kutoka nje.

## **Mafanikio ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2014/15**

10. Mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2014/15 ni pamoja na yafuatayo:

- i. Kuandaa Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015 na kupitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuanza kutumika rasmi tarehe 01 Julai, 2015. Utekelezaji wa Sheria hii unatarajia kuboresha usimamizi wa matumizi ya fedha za umma na hatimaye kuimarika kwa nidhamu ya utekelezaji wa bajeti ya Serikali;
- ii. Kujenga barabara za kupunguza msongamano wa magari katika jiji la Dar es Salaam;
- iii. Kuongeza bajeti ya sekta ya kilimo, ikijumuisha fedha za ruzuku ya pembejeo (mbolea, mbegu bora na dawa za mimea) kutoka shilingi bilioni 866.9 mwaka 2012/13 hadi shilingi bilioni 1,084.7 mwaka 2014/15;
- iv. Kukamilisha ujenzi wa bomba la gesi Mtwara – Dar es Salaam pamoja na mtambo wa kuzalisha umeme wa gesi – Kinyerezi I wa MW 150;
- v. Kuendelea kujenga na kukarabati miundombinu ya maji ambayo imeongeza idadi ya watu wanaopata maji safi na salama vijijini kutoka asilimia 51 mwaka 2013/14 hadi asilimia 60 ikilinganishwa na lengo la asilimia 57 kwa mwaka 2014/15;
- vi. Kuongeza idadi ya wanafunzi wa elimu ya juu wanaofaidika na mikopo; na

- vii. Kugharamia uchaguzi wa serikali za mtaa wa mwaka 2014 pamoja na Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015.

### **Changamoto za Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2014/15**

11. Licha ya mafanikio yaliyopatikana katika sekta mbalimbali za kijamii na kiuchumi, utekelezaji wa bajeti ya Serikali ya mwaka 2014/15 ulikabiliwa na changamoto zifuatazo:

- i. ukwepaji wa kodi;
- ii. mwitikio hasi kwenye matumizi ya mashine za kielektroniki (EFDs);
- iii. kuibuka kwa masharti mapya katika utoaji wa fedha za misaada na mikopo ya kibajeti;
- iv. Kuongezeka kwa malimbikizo ya madai ya makandarasi, watoa huduma na watumishi;
- v. Kuongezeka kwa matumizi ya Serikali kusikowiana na hali halisi ya upatikanaji wa mapato;
- vi. Mazingira magumu ya ukusanyaji wa kodi katika sekta isiyo rasmi; na
- vii. Ufanisi duni wa baadhi ya mashirika unaolazimu kuendelea kupata ruzuku ya mishahara na uendeshaji kutoka serikalini.

### **Hatua za Kukabiliana na Changamoto za Utekelezaji wa Bajeti 2014/15**

12. Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kukabiliana na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa bajeti. Baadhi ya hatua hizo ni pamoja na:

- i. kusimamia dhana ya kulipa kodi kwa hiari na uwajibikaji kwa watumishi wasio waadilifu;
- ii. mpango wa kutoa mashine za EFDs na kudhibiti matumizi ya mfumo huo;
- iii. kuendelea na majadiliano baina ya serikali na Washirika wa Maendeleo ili kupata fedha za misaada na mikopo kama ilivyopangwa;
- iv. mafungu kutoingia mikataba ya huduma bila kuzingatia uwezo wa bajeti na upatikanaji wa fedha;
- v. kupunguza matumizi yasiyo ya lazima;
- vi. kuendelea na utekelezaji wa programu mbalimbali za kurasimisha shughuli za sekta isiyo rasmi; na
- vii. Serikali inakusudia kufanya marekebisho makubwa kwa mashirika ya umma ili yaweze kujiendesha kibiashara bila kutegemea ruzuku ya Serikali.

### **Utekelezaji wa Bajeti ya Nusu Mwaka ya 2015/16**

13. Katika mwaka 2015/16, Serikali ilipanga kukusanya na kutumia kiasi cha shilingi bilioni 22,495.5. Katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2015, mapato yote ya Serikali yalikuwa jumla ya shilingi bilioni 10,237.7 ikiwa ni sawa na asilimia 88.8 ya makadirio ya nusu mwaka. Aidha, hadi kufikia Desemba 2015, Serikali imetoa mgao wa matumizi wenye thamani ya shilingi bilioni 10,312.4 sawa na asilimia 89 ya lengo

la shilingi bilioni 11,531.1 katika kipindi hicho. Kati ya kiasi kilichotolewa, shilingi bilioni 8,181.5 zilikuwa ni matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 2,130.9 ni matumizi ya maendeleo.

### **Mafanikio ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2015/16**

14. Mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha nusu mwaka 2015/16 ni pamoja na yafuatayo:

- i. Ongezeko la makusanyo ya mapato ya kodi;
- ii. Kufanikisha Uchaguzi Mkuu kwa kutumia mapato ya ndani;
- iii. Kuongezeka kwa wanafunzi wanaofaidika na mikopo ya elimu ya juu
- iv. Kuanza utekelezaji wa elimu msingi bila malipo;
- v. Kuanza kulipa madai ya wakandarasi na madai ya mikataba ya vifaa vya ulinzi na usalama;
- vi. Utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mapato ya ndani (kama vile Wakala wa Umeme Vijijini, Wakala wa Barabara, Kinyerezi II pamoja na miradi yenye vyanzo vya mapato kama Mfuko wa Reli, Mfuko wa Maji, na
- vii. Ulipaji wa mishahara ya watumishi wa Serikali kwa wakati.

### **Changamoto za Utekelezaji wa Bajeti Mwaka 2015/16**

15. Licha ya mafanikio yaliyopatikana katika sekta mbalimbali za kijamii na kiuchumi, utekelezaji wa bajeti ya Serikali nusu ya kwanza ya mwaka 2015/16 ulikabiliwa na changamoto zifuatazo:

- i. Ukwepaji wa Kodi kwa wafanyabiashara wasio waadilifu;
- ii. Mwitikio hasi kwenye matumizi ya mashine za kielektroniki (EFDs);
- iii. Kuongezeka kwa matumizi ya Serikali kusikouwiana na hali halisi ya upatikanaji wa mapato;
- iv. Mazingira magumu ya ukusanyaji wa kodi katika sekta isiyo rasmi; na
- v. Ufanisi duni wa baadhi ya mashirika unaolazimu kuendelea kupata ruzuku ya mishahara na uendeshaji kutoka serikalini.

### **Hatua za Kukabiliana na Changamoto za Bajeti Mwaka 2015/16**

16. Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kukabiliana na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa bajeti. Baadhi ya hatua hizo ni pamoja na:

- i. kusimamia dhana ya kulipa kodi kwa hiari na uwajibikaji kwa wafanyabishara wasio waadilifu;
- ii. mpango wa kutoa mashine za EFDs na kudhibiti matumizi ya mfumo huo;
- iii. kuendelea na majadiliano baina ya Serikali na Washirika wa Maendeleo ili kupata fedha za misaada na mikopo kama ilivyopangwa;
- iv. kupunguza matumizi yasiyo ya lazima na kuimarisha usimamizi wa ukusanyaji wa mapato;

- v. kuendelea na utekelezaji wa programu mbalimbali za kurasimisha shughuli za sekta isiyo rasmi; na
- vi. Serikali inakusudia kufanya marekebisho makubwa kwa mashirika ya umma ili yaweze kujiendesha kibiashara bila kutegemea ruzuku ya Serikali.

## **MAMBO MUHIMU KATIKA MWONGOZO WA MWAKA 2016/17**

17. Katika uandaaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka fedha 2016/17 Serikali inatarajia kusimamia mambo muhimu kama ifuatavyo:

### **a) Shabaha za Uchumi Jumla**

18. Shabaha na malengo ya uchumi jumla katika kipindi cha 2016/17 – 2020/21 ni kama ifuatavyo:-

- i. Pato Halisi la Taifa kukua kwa asilimia 7.0 mwaka 2015, asilimia 7.2 mwaka 2016, na kuendelea kuongezeka hadi wastani wa asilimia 8 katika kipindi cha muda wa kati kwa kutumia takwimu zilizorekebishwa za mwaka wa kizio wa 2007;
- ii. Kuendelea kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei na kuhakikisha kuwa unabaki kwenye wigo wa tarakimu moja kufikia asilimia 6.0 Juni 2016 na kubaki kati ya asilimia 5 na asilimia 8 katika kipindi cha muda wa kati;
- iii. Mapato ya ndani ikijumuisha mapato ya Halmashauri kufikia asilimia 14.8 ya Pato la Taifa mwaka 2016/17, asilimia 15.1 mwaka 2017/18, na asilimia 16.3 mwaka 2019/20;
- iv. Mapato ya kodi kufikia asilimia 13.2 ya Pato la Taifa mwaka 2016/17, asilimia 13.5 ya Pato la Taifa mwaka 2017/18 na kufikia asilimia 14.4 ya Pato la Taifa ifikapo mwaka 2019/20;
- v. Matumizi ya Serikali yanatarajiwa kupungua kutoka asilimia 23.9 ya Pato la Taifa mwaka 2015/16 hadi asilimia 21.5 mwaka 2016/17 kufuatia kukamilika kwa uchaguzi mkuu;
- vi. Kupunguza nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) kutoka asilimia 4.2 mwaka 2015/16 na kuendelea kupungua hadi chini ya asilimia 3.0 katika kipindi cha muda wa kati;
- vii. Kasi ya ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) kuwa asilimia 16.0 Juni 2016 na kupungua kufikia asilimia 15.6 Juni 2017 na kubakia katika kiwango cha wastani wa zaidi ya asilimia 14.0 katika kipindi cha muda wa kati sambamba na lengo la kupunguza mfumuko wa bei;
- viii. Nakisi katika urari wa malipo ya kawaida kuwa asilimia 9.4 ya Pato la Taifa mwaka 2015/16 na kuendelea kupungua hadi chini ya wastani wa asilimia 8 katika kipindi cha muda wa kati; na

- ix. Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne.

**b) Misingi ya Mpango na Bajeti**

19. Misingi ya Mpango na Bajeti ya Serikali katika kipindi cha muda wa kati (2016/17-2018/19) ni pamoja na:-

- i. Amani, usalama, na utulivu wa ndani na nchi jirani vitaendelea kuimarishwa na kudumishwa;
- ii. Viashiria vya uchumi jumla na maendeleo ya jamii kama vile Pato la Taifa, biashara ya nje, ujazi wa fedha, mapato na matumizi na viashiria vya huduma za jamii vitaendelea kuimarika;
- iii. Sera za fedha zitaendelea kuimarishwa ili ziendane na sera za bajeti zitakazosaidia kupunguza mfumuko wa bei na tofauti kati ya riba za amana na za mikopo;
- iv. Kuendelea kuimarika na kutengemaa kwa uchumi wa dunia;
- v. Bei za mafuta katika soko la dunia zitaendelea kuwa nzuri; na
- vi. Hali nzuri ya hewa nchini na katika nchi jirani.

**3.0 MABORESHO YA MFUMO WA BAJETI**

20. Serikali imefanya maboresho mbalimbali katika bajeti ili kufanya usimamizi wa bajeti unakuwa na ufanisi zaidi, kuongeza uwajibikaji na uwazi. Maboresho makubwa ni pamoja na kuandaliwa na kupitishwa kwa Sheria ya Bajeti.

**3.1 Sheria ya Bajeti**

21. Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015 ilipitishwa tarehe 11 Mei, 2015 na kuanza utekelezaji wake tarehe 1 Julai 2015. Dhumuni la msingi la Sheria hii ni kuhakikisha kunakuwa na usimamisi madhubuti wa bajeti na uwajibikaji. Hivyo basi, Maafisa Masuuli wote wanatakiwa kuzingatia Sheria hii na kanuni zake wakati wa kuandaa na kutekeleza mipango na bajeti. Serikali itaendelea kutoa elimu ya Sheria ya Bajeti kwa wadau wa ngazi zote.

**4.0 MAANDALIZI YA MIPANGO NA BAJETI ZA TAASISI**

**4.1 Kamati za Bajeti**

22. Kwa mujibu wa kifungu cha 18 cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015 na Kanuni zake, Maafisa Masuuli wanatakiwa kuunda Kamati za Bajeti za taasisi zao na kusaidia katika maandalizi ya mpango na bajeti. Majukumu ya Kamati za Bajeti yameainishwa katika Kanuni ya 17(3) ya Sheria ya Bajeti. Kamati pia zinatakiwa kutekeleza majukumu mengine kama yalivyoainishwa katika Mwongozo huu, Waraka wa Msajili wa Hazina na nyaraka nyingine za Serikali.

#### **4.2 Ratiba ya Maandalizi ya Mpango na Bajeti**

23. Mara baada ya kutolewa kwa Mwongozo wa Mpango na Bajeti na viwango vya ukomo wa bajeti kwa mwaka wa fedha wa 2016/17, Wizara, Idara zinazojitegemea, na Wakala wa Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mashirika ya Umma zitapaswa kuandaa mipango yao ya muda wa kati (MTEFs) na kuiwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango kabla ya wiki ya tatu ya mwezi Februari, 2016. Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaagizwa kuandaa mipango na makadirio ya bajeti na kuziwasilisha kwa mamlaka husika na Kamati za Bajeti kwa ajili ya majadiliano na kupata kibali kabla ya wiki ya kwanza ya mwezi Februari, 2016. Baada ya bajeti za Mamlaka za serikali za mitaa kuidhinishwa, zitawasilishwa Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya uchambuzi zaidi. Kati ya wiki ya tatu ya mwezi wa Machi, 2016 na wiki ya kwanza ya mwezi wa Aprili, 2016 Wizara ya Fedha na Mipango itaunganisha bajeti za mafungu na kuziwasilisha kwenye Kamati za kudumu za Bunge za kisekta kwa ajili ya kufanya uchambuzi na kuandaa mapendekezo yatakayowasilishwa bungeni. Makadirio ya bajeti yatawasilishwa bungeni kwa ajili ya kujadiliwa na kupitishwa kuanzia wiki ya pili ya mwezi Aprili hadi wiki ya nne ya mwezi Juni, 2016. Utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2016/17 utaanza tarehe 1 Julai, 2016.

#### **4.3 Mchakato wa Uchambuzi wa Bajeti**

24. Uchambuzi wa kitaalam utafanywa kwa pamoja baina ya Wizara ya Fedha na Mipango; Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora; Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Ofisi ya Msajili wa Hazina na wadau wengine. Kwa mujibu wa Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015, kifungu cha 22(1) na kifungu cha 68(a-e), mashirika yote ya umma yanaagizwa kuwasilisha makadirio yao ya bajeti Wizara ya Fedha na Mipango kupitia kwa wizara mama kwa ajili ya uchambuzi na mapendekezo ya marekebisho. Wizara zinapaswa kuzielekeza taasisi zilizo chini yao kuandaa bajeti zao kulingana na maelekezo ya Mwongozo huu. Hali kadhalika, Ofisi ya Rais-TAMISEMI itazisaidia Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuzingatia maelekezo yaliyomo katika Mwongozo huu.

25. Kulingana na maelekezo hayo ya uchambuzi wa bajeti, Wizara, Idara zinazojitegemea, na Wakala wa Serikali, Sekretariati za Mikoa, Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Mashirika ya Umma zinapaswa kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango na Ofisi ya Rais-TAMISEMI nakala mbili (2) ngumu na laini za makadirio ya bajeti zao kwa ajili ya uchambuzi wa kitaalamu kabla ya kuwasilisha nakala ya makadirio ya bajeti iliyosainiwa kwa mamlaka hizo. Ili kuweka ufafanuzi mzuri na wa uwazi katika zoezi zima, mchakato wa uchambuzi utaendeshwa kwa kuzingatia yafuatayo:

- a) Kufanya mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka uliopita (2014/15);
- b) Kufanya mapitio ya mapato na matumizi ya kipindi cha nusu mwaka wa 2015/16, changamoto na hatua zilizochukuliwa kukabiliana nazo;

- c) Kuzingatia kanuni za uandaaji wa makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka 2016/17;
- d) Kuzingatia ukomo wa bajeti uliotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango;
- e) Kuwasilisha makadirio ya bajeti yalioandaliwa kwa mfumo wa utengaji bajeti wa kimkakati (Strategic Budget Allocation System – SBAS) unaotumiwa na Wizara, Idara zinazojitegemea, na Wakala wa Serikali, Sekretariati za Mkoa, na vile vile kwa kutumia mfumo wa uandaaji wa mpango na utoaji wa taarifa (PlanRep) unaotumiwa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa; na
- f) Kuzingatia maelekezo yaliyotolewa katika Mwongozo huu, Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015 na kanuni zake, Sheria ya Msajili wa Hazina, pamoja na nyaraka na miongozo mingine ya serikali.

#### **4.4 Uingizaji wa Takwimu za Bajeti Katika Mfumo wa Malipo**

26. Kulingana na ratiba ya maandalizi na uchambuzi wa bajeti, Maafisa Masuuli wote wanatakiwa kutekeleza yafuatayo:

- a) Kukamilisha kwa wakati zoezi la kuingiza takwimu za bajeti kwenye mfumo wa malipo na kuhakikisha usahihi wake;
- b) Kuzingatia mfumo wa kimataifa wa mwaka 2014 wa takwimu za kifedha za serikali na za miradi (GFS Codes) kama ilivyotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango;
- c) Kutumia vipimo sahihi hususani vinavyotolewa katika mfumo wa SBAS na PlanRep; na
- d) Kuweka makadirio sahihi ya gharama za kodi ya pango, umeme, maji na simu.

## **5.0 MAELEKEZO YA MAANDALIZI YA BAJETI**

### **5.1 Mfumo wa Mapato na Matumizi Katika Kipindi cha Muda wa Kati**

27. Kwa kuzingatia sera za uchumi pamoja na misingi na sera za bajeti kwa mwaka 2016/17, Sura ya Bajeti inaonesha kuwa jumla ya Shilingi bilioni 22,991.5 zinatarajiwa kukusanywa na kutumika katika kipindi hicho. Jumla ya mapato ya ndani ikijumuisha mapato ya Halmashauri yanatarajiwa kuwa Shilingi bilioni 15,801.2. Kati ya kiasi hicho, mapato ya kodi ni Shilingi bilioni 14,106.6, mapato yasiyo ya kodi ni Shilingi bilioni 1,110.2 na Shilingi bilioni 584.4 ni mapato ya Halmashauri. Serikali inategemea kupata kiasi cha Shilingi bilioni 2,107.4 ikiwa ni misaada na mikopo kwa ajili ya kugharamia Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Mwaka 2016/17. Mchanganuo wa vyanzo vya mapato ya ndani ambavyo vimebainishwa hadi sasa kwa mwaka 2016/17 ni kama inavyoonekana katika **Kiambatisho namba 1**

28. Kutokana na changamoto zilizotokana na utaratibu wa Misaada ya Kibajeti

(General Budget Support), Serikali itaingiza michango hiyo katika bajeti pindi itakapo thibitishwa na kila Mshirika wa Maendeleo. Vile vile, Serikali inatarajia kukopa kiasi cha shilingi bilioni 1,782.3 kama mikopo ya nje yenye masharti ya kibiashara ili kupunguza nakisi ya bajeti.

29. Kwa upande wa matumizi, katika mwaka 2016/17 Serikali inapanga kutumia jumla ya Shilingi bilioni 22,991.5 kwa matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 16,809.2 zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ikijumuisha Shilingi bilioni 6,651.5 kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Serikali. Aidha matumizi ya maendeleo yatakuwa Shilingi bilioni 6,182.2 ambapo kiasi cha Shilingi bilioni 4,810.1 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 1,372.1 ni fedha za nje.

### **5.2 Viwango vya Ukomo wa Bajeti Katika Kipindi cha Muda wa Kati**

30. Viwango vya ukomo wa bajeti kwa ajili ya maandalizi ya bajeti vitatolewa kwa mafungu yote kwa kuzingatia sura ya bajeti. Hivyo, ukomo wa bajeti kwa kila fungu utatolewa kwa kuzingatia vigezo vya ugawaji rasilimali. Aidha, hakutakuwa na nyongeza ya ukomo wa bajeti nje ya viwango vitakavyotolewa isipokuwa kwa mambo yaliyoainishwa kwenye Kifungu Na. 37 cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015. Kwa msingi huo, Maafisa Masuuli wanatakiwa kuzingatia ukomo wa viwango vya bajeti vilivyoidhinishwa kwa mwaka 2016/17.

### **5.3 Mikakati ya Kuongeza Mapato**

31. Serikali inatarajia kuweka mikakati na hatua za kuongeza na kuimarisha ukusanyaji wa mapato. Mapato yote yatakusanywa na Wizara ya Fedha na Mipango. Hivyo basi, Maafisa Masuuli wa Wizara, Idara zinazojitegemea, Taasisi na Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, na Mamlaka za Serikali za Mitaa watatakiwa kuwasilisha mapato yote yatakayokusanywa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali na yatagawiwa kulingana na bajeti zitakazoidhinishwa katika mafungu hayo. Hatua hii inazihusu pia taasisi zote za umma zinazotumia utaratibu wa 'Retention' kwa sasa. Ili kutimiza lengo hili, Maafisa Masuuli wote wanaelekezwa kuweka mazingira wezeshi katika kufanikisha ukusanyaji wa mapato kwa kufanya yafuatayo:

- (i) Kuainisha vyanzo vyote vya mapato kama moja ya mkakati wa kuboresha ukusanyaji wa mapato;
- (ii) Kutumia mfumo wa ukadiriaji wa majengo kwa mkupuo (*mass valuation*) kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zote katika ukusanyaji wa kodi za majengo. Aidha, Majengo ambayo hayajafanyiwa uthamini yatozwe kodi kwa viwango vinavyofanana kwa majengo ya kila kundi. Zoezi hili lifanyike kwa kipindi cha mpito wakati zoezi la uthamini wa majengo hayo likikamilishwa;
- (iii) Kupima na kuanisha matumizi ya ardhi kwa ajili ya utoaji wa Hati miliki ya ardhi;

- (iv) Kuboresha mazingira ya urasimishaji wa biashara ili kupanua wigo wa kodi;
- (v) Kupitia upya ada, ushuru na tozo ili kuzirekebisha ziendane na viwango vya soko katika kutoa huduma za umma;
- (vi) Kuhakikisha taasisi zote umma zinatumia mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa kodi, ada, ushuru na tozo ili kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato;
- (vii) Kuingia mikataba na wazabuni, makandarasi na watoa huduma wanaotumia mashine za kielektroniki;
- (viii) Kufanya mapitio ya mikataba yote iliyopewa misamaha ya kodi ili kutathmini faida zake na kujipanga upya; na
- (ix) Kutoingia mikataba inayohusisha misamaha ya kodi bila idhini ya Waziri wa Fedha na Mipango.
- (x) Maeneo

32. Pamoja na hatua zilizotajwa hapo juu, Maafisa Masuuli wanatakiwa kuhakikisha kuwa makadirio na makusanyo ya mapato yanawasilishwa katika utaratibu uliowekwa. Kwa mujibu wa Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015, Maafisa Masuuli wote wanatakiwa kuhakikisaha kwamba mapato yote yanawasilishwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.

#### **5.4 Vigezo vya Kugawa Rasilimali**

33. Makadirio ya matumizi ya Serikali yamegawanyika katika sehemu mbili ambazo ni; matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo.

##### **5.4.1 Matumizi ya Kawaida**

###### **a) Mishahara**

34. Bajeti ya mishahara itazingatia watumishi waliopo, upandishwaji vyeo, watumishi wapya, makato na michango ya kisheria. Katika maandalizi ya bajeti ya mishahara, Maafisa Masuuli wanatakiwa kuzingatia maelekezo na nyaraka zilizotolewa na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora. Taasisi na Wakala za Serikali zizingatie maelekezo yaliyotolewa na Ofisi ya Msajili wa Hazina. Hivyo, Maafisa Masuuli wanatakiwa kuzingatia yafuatayo:

- (i) Kutumia taarifa za rasilimali watu zilizohakikiwa katika uandaaji wa makadirio ya bajeti za mishahara kwa watumishi waliopo. Aidha, uandaaji wa bajeti ya watumishi wapya uzingatie kibali kutoka Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora;
- (ii) Kutumia Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Rasilimali Watu - HCMS katika kuandaa bajeti ya mishahara;

- (iii) Kutambua mahitaji ya ikama kwa kufanya tathmini ya watumishi waliopo kwa kulinganisha na kibali kilichotolewa ili kuwasilisha taarifa ya ikama Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora kupitia Mfumo wa HCMIS;
- (iv) Bajeti kwa ajili ya posho za kukaimu nafasi za uongozi zinazosubiri uteuzi zitengwe katika bajeti ya mishahara. Aidha, posho za kukaimu nafasi za uongozi zinazotokana na ugonjwa, likizo na safari zitaendelea kukasimiwa katika bajeti ya matumizi mengineyo;
- (v) Michango ya kisheria na ya kiinua mgongo kwa watumishi wenye ajira za mikataba ikadiriwe kwa usahihi; na
- (vi) Kufanya ukaguzi wa rasilimali watu ili kupata uwiano na mgawanyo sahihi wa watumishi.

35. Ikumbukwe kuwa katika mwaka wa fedha 2016/17 kipaumbele cha ajira mpya kitatolewa katika sekta zenye upungufu wa watumishi. Sekta hizo ni: elimu (walimu wa sayansi, hisabati, kingereza na fundi sanifu wa maabara); afya; kilimo na nishati (mafuta na gesi). Ajira mpya katika sekta nyingine zitategemea uwepo wa rasilimali fedha na nafasi za kazi.

#### **Mfuko Mkuu wa Serikali (CFS)**

36. Bajeti kutoka katika Mfuko Mkuu wa Serikali itatumika kwa ajili ya kulipa Deni la Taifa na michango ya watumishi katika mifuko ya hifadhi za jamii. Aidha, Kifungu Na. 47 cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015 kinaelekeza kuwa bajeti ya Mfuko Mkuu wa Serikali itatengwa Wizara ya Fedha na Mipango.

#### **Mfuko wa Dharura**

37. Serikali imeanzisha Mfuko wa Dharura kwa ajili ya kugharamia mahitaji ya dharura kama ilivyoainishwa katika Kifungu Na. 35 cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015. Aidha, Kanuni Na. 23 ya Sheria ya Bajeti inaelekeza kuwa bajeti ya Mfuko huo itakuwa ni asilimia moja ya bajeti yote na itatengwa Wizara ya Fedha na Mipango.

#### **Matumizi Mengineyo (OC)**

38. Maafisa Masuuli wote wanaelekezwa kuhakikisha wanatenga fedha za kutosha kwa ajili ya matumizi yasiyoepukika pamoja na majukumu ya msingi katika mafungu yao. Vile vile, wanaelekezwa kufanya mapitio ya mpango mkakati ili kuiwianisha na Mpango wa Maendeleo wa 2016/17, Ilani ya Chama Tawala 2015 na mipango mingine ya kitaifa. Pia, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa wahakikishe wanandaa Mpango Kabambe na *Profiles* na kuziwianisha na mpango mkakati ili kuondokana na tatizo la makazi holela (unplanned settlements).

### **Ruzuku kwa Serikali za Mitaa**

39. Serikali itaendelea kutoa ruzuku kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha zinaboresha utoaji wa huduma katika maeneo yao. Ruzuku hizo zitatolewa kwa mfumo wa ruzuku jumla, ruzuku ya maendeleo ya Serikali za Mitaa pamoja na mifumo mingine ya fedha za maendeleo. Ukomo wa bajeti unakadiriwa kwa kutumia matokeo ya upimaji wa utendaji kazi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa na vigezo kanuni vya ugawaji wa rasilimali. Katika uandaaji wa mipango na bajeti, Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaelekezwa kuzingatia mambo yafuatayo:

- (i) 'Capitation' kwa shule za msingi itaendelea kuwa shilingi 10,000 kwa mwanafunzi kwa mwaka, hii inajumuisha wanafunzi wa shule za awali na maalum. Aidha, asilimia 40 ya fedha za 'capitation' zitaendelea kutumika kwa ajili ya ununuzi wa vitabu katika utaratibu wa ununuzi wa pamoja 'centrally' na kiasi kinachobaki cha asilimia 60 kitatumwa moja kwa moja kwenye akaunti za shule husika;
- (ii) 'Capitation' kwa shule za sekondari itaendelea kuwa shilingi 25,000 kwa mwanafunzi wa kutwa na bweni kwa mwaka. Asilimia 50 ya fedha za 'capitation' zitaendelea kutumika kwa ajili ya ununuzi wa vitabu katika utaratibu wa ununuzi wa pamoja na kiasi kinachobaki cha asilimia 50 kitatumwa moja kwa moja kwenye akaunti za shule husika;
- (iii) Kigezo cha kutenga fedha kwa ajili ya chakula cha wanafunzi kitaendelea kuwa shilingi 540,000 kwa mwaka (shilingi 2,000 x 270 school days) kwa mwanafunzi aliyesajiliwa kwenye shule za bweni za msingi na sekondari; na
- (iv) Uandaaji wa bajeti za mitihani ya shule za msingi na sekondari uzingatie viwango halisi vya mahitaji.

### **5.4.3 Maeneo ya Kipaumbele 2016/17**

40. Mpango wa maendeleo wa Taifa wa 2016/17 unaelekeza maeneo yafuatayo ya kipaumbele:

#### **Viwanda**

41. Katika mwaka 2016/17 aina ya viwanda vitakavyopewa kipaumbele ni pamoja na: viwanda wambavyo sehemu kubwa ya malighafi yake inapatikana nchini, hususani kwenye sekta za kilimo, mifugo, uvuvi, madini na miliasili nyingine; viwanda vya kuzalisha bidhaa zinazotumiwa na watu wengi nchini, kama vile nguo, viatu na mafuta ya kupikia; na viwanda vinavyotumia teknolojia ya kati na kuajiri watu wengi.

#### **Miradi Mikubwa ya Kielelezo**

42. Miradi mikubwa ya kielelezo (flagship projects) ni miradi mikubwa itakayobainishwa ili kusisimua ukuaji wa uchumi na hivyo kutoa matokeo mapana yatakayokuwa kielelezo cha mafanikio ya Mpango. Baadhi ya miradi hiyo ni

uendelezaji wa maeneo maalum ya uwekezaji (SEZ) ya Bagamoyo, Mtwara, Kigoma na Kurasini. Mji wa kilimo Mkulazi, kiwanda cha chuma cha Liganga, ujenzi wa reli ya kati, kujenga msingi wa kuzalisha mitambo, nyenzo na malighafi za uzalishaji, kuimarisha huduma za usafiri za abiria na mizigo katika maziwa makuu, na Bahari ya Hindi na kuimarisha Shirika la Ndege Tanzania nk.

### **Maeneo Wezeshi kwa Maendeleo ya Viwanda**

43. Maeneo wezeshi kwa amaendeleo ya viwanda yatayoendelea kutekelezwa ni pamoja na: Miundombinu ya nishati, Reli, barabara, viwanja vya ndege, bandari, maji (kwa mahitaji ya viwanda na umwagiliaji) na mkongo wa Taifa wa mawasiliano.

### **Kufungamanisha Maendeleo ya Viwanda na Watu**

44. Serikali itaweka msisitizo mkubwa katika kufungamanisha maendeleo ya viwanda na maendeleo ya watu. Maeneo mahususi yanayopendekezwa kutekelezwa ni pamoja na: kuhakikisha usalama wa chakula, afya ikiwemo kuimarisha mfumo wa upataikanaji wa dawa kwa wananchi, kuimarisha upatikanaji wa elimu ikiwa ni pamoja na kutoa elimu ya msingi bila malipo na kuhakikisha ubora wa elimu kwa kuendelea kutoa mafunzo kwa waalimu walio kazini, kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji, usimamizi wa upatikanaji wa maji safi na maji taka (kwa mahitaji wa viwanda na umwagiliaji nk)

### **Maeneo Mengine**

45. Mapendekeo ya muelekeo wa Mpango wa maendeleo wa Taifa wa 2016/17 unabainisha maeneo mengine muhimu kwa ukuaji wa uchumi na ustawi wa Taifa. Maeneo hayo ni pamoja na Utalii, misitu na wanyama pori; Madini; Hali ya Hewa; Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa; na Utawala Bora. Maeneo haya ni muhimu katika kuchochea biashara ya Kimataifa na hivyo kuongeza mapato ya fedha za kigeni.

#### **5.4.4 Bajeti ya Maendeleo**

46. Wizara, Idara zinazojitegemea, Taasisi na Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaelekezwa kuzingatia maeneo ya vipaumbele kama yalivyoainishwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2016/17 na kutumia Mwongozo wa Uandaaji wa Miradi ya Kimkakati (PIM-OM). Aidha, ruzuku kwa ajili ya bajeti ya Maendeleo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa (Local Government Development Grant) zitatolewa kwa kuzingatia mapitio ya vigezo vilivyopo kwenye 'Local Government Implementation Guide'. Maafisa Masuuli wanatakiwa kuhakikisha kuwa:

- a) Kipaumbele kinatolewa kwa miradi ya miundombinu inayoendelea ili ikamilishwe kabla ya kuanza kutekeleza miradi mipya;
- b) Kulipa madeni ya makandarasi, wazabuni na watoa huduma;

- c) Ugawaji wa rasilimali utoe kipaumbele kwenye miradi ya kimkakati;
- d) Miradi mipya iwasilishwe Wizara ya Fedha na Mipango kwa uchambuzi;
- e) Miradi itakayotengewa fedha ni ile itakayokuwa na andiko la mradi, taarifa ya upembuzi yakinifu na taarifa ya tathmini ya kijamii na kimazingira; na
- f) Mikopo kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa miradi inayoendelea izingatie Sheria ya Mikopo na Dhamana Na. 30 ya mwaka 1974 na marekebisho yake ya mwaka 2004. Aidha, Mamlaka za Serikali za Mitaa zizingatie Sheria ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa Na. 9 ya mwaka 1982 na marekebisho yake pamoja na Vifungu Na. 60(4) na 62(b) vya Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015.

47. Kwa upande wa fedha za maendeleo kutoka nje, Wizara, Idara zinazojitegemea, Taasisi na Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatakiwa kuandaa bajeti kwa kuzingatia ahadi zilizothibitishwa na Washirika wa Maendeleo pamoja na kuhakikisha kwamba:

- a) Mchango wa Serikali kwenye miradi ya ubia (counter fund) inatengewa bajeti;
- b) Miradi yote inayopata fedha za Washirika wa Maendeleo inajumuishwa katika bajeti ya Serikali; na
- c) Miradi yote inayopata fedha za Washirika wa Maendeleo na kuwasilishwa Wizara ya Fedha na Mipango iwe na mikataba.

## **6.0 MAMBO MENGINE YA KUZINGATIWA KATIKA UANDAAJI WA BAJETI**

### **6.1 Kudhibiti Ulimbikizaji wa Madeni**

48. Ili kuepuka ulimbikizaji wa madeni, Maafisa Masuuli wanapaswa kuzingatia Kifungu cha 52(1) cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015 pamoja na Waraka Na. 4 wa Mlipaji Mkuu wa Serikali wenye Kumb. Na. CBA.187/355/01/15 wa tarehe 31 Disemba 2014. Kutokana na hali hiyo, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuchukua hatua zifuatazo:

- a) Kuweka kipaumbele katika utengaji wa fedha za kulipia madeni yaliyohakikiwa;
- b) Kuhakikisha kwamba hakuna madeni mapya yanayozalishwa;
- c) Kubainisha madeni yaliyopo na kuhakikisha yanaingizwa kwenye hesabu za serikali; na
- d) Kuingiza matumizi yote kwenye mfumo wa malipo wa IFMS.

### **6.2 Madeni yatokanayo na dhamana za Serikali kwa Mashirika**

49. Katika kusimamia na kudhibiti madeni yatokanayo na dhamana za serikali kwenye mashirika ya umma, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kufanya ufuatiliaji wa karibu wa mikataba inayoweza kusababisha hasara na madeni kwenye mashirika yaliyo chini yao.

### **6.3 Hatua za kudhibiti matumizi**

50. Maafisa Masuuli wanapaswa kuendelea kutekeleza hatua za kubana matumizi katika maeneo yote yaliyopo chini yao ikiwa ni pamoja na yafuatayo:

- a) Kupunguza gharama na matumizi yasiyokuwa ya lazima ikiwemo sherehe za kitaifa, posho za vikao, uchapishaji wa fulana, kofia, mikoba, diary, kalenda, safari za nje, na mafunzo ya muda mfupi, kama ilivyoelekezwa na serikali ya Awamu ya Tano, na badala yake fedha hizo zielekezwe kwenye shughuli za kipaumbe katika taasisi husika;
- b) Kuhakikisha mikutano yote ikiwa ni pamoja na mikutano ya bodi, mafunzo na semina inatumia kumbi za Serikali na Taasisi za Umma;
- c) Kutoa kipaumbele kwa Taasisi za Umma katika kununua huduma kama vile bima, usafirishaji wa barua, mizigo na vifurushi (courier), matangazo na usafiri;
- d) Kuzingatia maelekezo ya Mlipaji Mkuu wa Serikali wakati wa uuzaji au uondoshaji wa mali chakavu katika idara za Serikali, taasisi na mashirika ya umma;
- e) Kuhakikisha Mashirika ya umma yaliyoundwa kwa lengo la kujiendesha kibiashara, yanajiendesha kwa faida bila kutegemea ruzuku ya Serikali. Mashirika hayo ni pamoja na TANESCO, TAZARA, TRL, ATCL, RAHCO, TEMESA, Wakala wa Vipimo (WMA), na Bodi ya Mazao Mchanganyiko;
- f) Kufanya mapitio ya taratibu za ununuzi wa chakula cha wanafunzi na wafungwa kwa kujumuisha hatua zinazopunguza gharama za ununuzi kama vile kutumia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA), Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko, na wazalishaji kwenye masoko yaliyopo vijijini;
- g) Kudhibiti matumizi ya umeme, simu na maji ikiwa ni pamoja na kutumia teknolojia inayobana matumizi ya nishati na kuhakikisha fedha zinazotengwa kwa ajili ya kulipia Ankara hizo zinatumika kama ilivyokusudiwa;
- h) Kufunga mita za maji na umeme zinazotumia mfumo wa malipo kabla (pre-paid meters) kama vile LUKU ili kudhibiti matumizi ya huduma hizo;
- i) Kufanya ukaguzi wa mara kwa mara katika matumizi ya umeme, maji na simu ili kudhibiti matumizi yasiyokuwa ya lazima;
- j) Kudhibiti ulipaji wa mishahara kwa kulipa watumishi wanaostahili na waliopo kwenye vituo vya kazi. Aidha Wizara ya Fedha na Mipango itafanya sensa ya watumishi wote ili kuondokana na watumishi wanaolipwa bila kustahili;
- k) Kuhakikisha matumizi sahihi ya LPO zinazotolewa kupitia mfumo wa malipo wa IFMS ili kudhibiti ulimbikizaji wa madeni;
- l) Kuendelea na ulipaji wa madeni ya kimikataba kwa makandarasi na watoa huduma baada ya kufanyiwa uhakiki na Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali kwa kuzingatia waraka Na. 4 wa Mlipaji Mkuu wa Serikali wenye Kumb. Na. CBA.187/355/01/15;
- m) Kutumia fursa za mikopo ya nyumba (mortgage facility) katika upatikanaji wa majemgo ya balozi na wawakilishi walioko nje ya nchi badala ya utaratibu wa kupanga;

- n) Kuendelea kufanya ununuzi wa bidhaa na huduma kwa pamoja/ wingi (in bulk) kutoka kwa wazalishaji au watengenezaji;
- o) Kutumia kikamilifu watumishi wa ndani na wastaafu wenye sifa stahiki katika maeneo waliyobobea badala ya kutumia wataalamu kutoka nje;
- p) Kudhibiti malipo ya stahili zikiwemo posho za wajumbe wa Bodi na watumishi wa Taasisi na mashirika ya umma, kwa kuzingatia Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001, Sheria zilizoanzisha Mashirika na Kanuni zao, pamoja na waraka wa Serikali Na. SHC/B.40/6/21 wa tarehe 28 Machi 1994;
- q) Kudhibiti safari za nje na ukubwa wa misafara kwa kuhakikisha inapata kibali kutoka Ikulu;
- r) Kuzingatia maelekezo ya Serikali yaliyotolewa kwa Waraka Na. CAC.134/213/01/K/114 wa tarehe 26 Septemba 2012, kuhusu kudhibiti ununuzi wa samani zinazoagizwa kutoka nje ya nchi;
- s) Kuhakikisha ununuzi wa magari unafanyika kwa pamoja kupitia GPSA baada ya kupata kibali cha ununuzi kutoka kwa Waziri Mkuu; na
- t) Kuwasilisha orodha ya magali, mashine na mitambo ikionesha aina, mwaka wa kutengenezwa, na hali yake (running condition).

#### **6.4 Kiwango cha kubadilisha fedha**

51. Takwimu zote za kifedha sharti ziwasilishwe kwa kutumia sarafu ya shilingi ya Tanzania. Hata hivyo, maeneo ya bajeti yanayotumia fedha za kigeni yatumie kiwango cha kubadilisha fedha cha shilingi za Tanzania 2,227.9 kwa Dola moja ya Marekani kwa mwaka 2016/17.

#### **6.5 Kujumuisha Masuala Mtambuka Katika Mpango na Bajeti**

52. Uandaaji wa bajeti ya mwaka 2016/17 unasisitiza kujumuisha masuala mtambuka katika utekelezaji wa mpango na bajeti. Ili kufanikisha lengo hili, kila Wizara, Idara zinazojitegemea, Taasisi na Wakala za Serikali, Mashirika ya Umma, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinasisitizwa kutenga fedha za kutekeleza vipaumbele kwenye masuala mtambuka. Vipaumbele hivyo ni pamoja na masuala ya kijinsia, ujenzi wa miundombinu rafiki kwa watu wenye ulemavu, lishe, mazingira, mabadiliko ya tabia nchi, virusi vya UKIMWI na UKIMWI, na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs).

#### **6.6 Utawala Bora na Utawala wa Sheria**

53. Serikali itaendelea kutekeleza maboresho mtambuka ambayo ni ya muhimu katika utawala bora, uboreshaji wa huduma na uwajibikaji ili kufikia malengo ya mpango wa maendeleo wa mwaka 2016/17. Maboresho haya yanajumuisha: Programu ya Sekta ya Umma (PSRP), Programu ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGRP), Programu ya Sekta ya Sheria (LSRP), Programu ya Sekta ya Fedha (PFMRP), Awamu ya Pili ya Maboresho ya Sekta ya Fedha (SGFRP), Uboreshaji wa Mazingira

ya Biashara (BEST), na Mkakati wa Taifa wa Kupambana na Rushwa (NACSAP). Maboresho mengine ya kuzingatia ni pamoja na udhibiti wa fedha haramu, ushirikiano wa uwazi Serikalini, mfumo wa nchi za kiafrika wa kujitathmini zenyewe (APRM), na mpango kazi wa taifa wa haki za binadamu 2013 – 2017. Hivyo, kila taasisi inapaswa kuzingatia majukumu yake na kuhakikisha inatenga fedha za kutekeleza maboresho yanayowahusu kwa ukamilifu.

### **6.7 Ajira na Uwezeshaji wa Kiuchumi**

54. Katika mwaka 2016/17, Serikali itaendelea kuhimiza jitihada za uwezeshaji kiuchumi kupitia Mfuko wa Uwezeshaji Kiuchumi, Mfuko wa Maendeleo ya Vijana, Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake, Mfuko wa Taifa wa Uwezeshaji Kiuchumi, Mfuko wa kuwawezesha kiuchumi wajasiliamali wadogo (SELF), na Mfuko wa Rais wa udhamini. Jitihada hizi zitawezesha uanzishwaji wa viwanda vya kusindika mazao ya kilimo na makampuni madogo yatakayozalisha ajira na kukuza kipato cha vijana na wanawake. Kadhalika, Serikali itaendelea kutekeleza programu ya kuzalisha ajira kwa vijana (2014/15 – 2016/17). Katika hali hii, kila Afisa Masuuli atapaswa kuainisha masuala yanayoweza kuzalisha ajira katika eneo analosimamia na kuwasilisha taarifa Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Kazi, Ajira, Vijana na Walemavu. Baada ya hatua hiyo, Ofisi ya Waziri Mkuu watafanya tathmini ya mifuko hiyo ya uwezeshaji kwa lengo la kuwianisha na kuboresha ufanisi wa shughuli za vijana na wanawake.

### **6.8 Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa**

55. Tanzania ni mwanachama wa jumuiya mbalimbali za kimataifa ikiwamo: Umoja na Mataifa (UN), Umoja wa Afrika (AU), Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC). Aidha, Tanzania imeridhia mikataba, itifaki na makubaliano mbalimbali ya kikanda na kimataifa. Kwa sasa SADC ni eneo huru la biashara ambalo liko kwenye mchakato wa kuanzisha umoja wa forodha. Vilevile, eneo la EAC ambalo ni soko la pamoja, limeridhia itifaki ya kuanzishwa kwa Umoja wa Fedha wa Afrika Mashariki. Serikali kwa kushirikiana na nchi wanachama wa EAC itaendelea kutekeleza mpango kazi wa miaka 10 wa kuelekea kwenye umoja wa fedha wa Afrika Mashariki. Katika kuwezesha ushiriki wa watanzania ili kupata faida zinazotarajiwa, kipaumbele kitawekwa kwenye majadiliano ya biashara na uwekezaji wa kimahusiano kwa Marekani, Umoja wa Ulaya, na ushirikiano wa utatu kati ya EAC, COMESA na SADC.

56. Kwa kuzingatia hali hiyo, kila Wizara, Idara zinazojitegemea, Taasisi na Wakala za Serikali, Mashirika ya Umma, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaagizwa kuzingatia yafuatayo:

- a) Kuwasilisha Hazina mihadi yote ya kuchangia michango ya taasisi za kimataifa na kikanda kwa ajili ya kuunganishwa sehemu moja, kutengewa fedha na kulipwa;

- b) Kuwianisha SADC na EAC na masuala mengine ya mtangamano kwenye mipango na bajeti zilizoko chini ya mamlaka zao;
- c) Kuhakikisha ufuatiliaji wa jumla na uratibu katika utekelezaji wa makubaliano mbalimbali katika sekta zao zilizosainiwa kati ya Tanzania na nchi nyingine pamoja na makubaliano ya kikanda na kimataifa;
- d) Kuhamasisha umma kwa kushirikiana na wadau wengine kuhusu fursa zilizopo katika EAC na SADC ili kunufaika nazo; na
- e) Kuchukua hatua za kisekta katika kutumia fursa za kifedha zilizopo katika ushirikiano wa kikanda na kimataifa.

### **6.9 Usimamizi wa Mali za Umma**

57. Maafisa Masuuli wanapaswa kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuhakiki, kupima, kuweka mipaka na kurasmisha umiliki wa mali za umma zikiwemo viwanja vya Serikali na maeneo ya wazi, maeneo ya viwanda, shule, vyyuo, vyyuo vikuu, maeneo ya jeshi na vyombo vya usalama, hospitali na zahanati, na mashamba ya umma ili yapewe hati miliki. Vilevile, wanapaswa kutenga fedha kwa ajili ya fidia ya ardhi na makazi kabla ya kupata ardhi ya uwekezaji kulingana na Sheria ya Ardhi Na. 4 ya 1999. Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kushirikiana na Halmashauri, kupitia Ofisi ya Rais – TAMISEMI atatoa hati miliki kwa taasisi ambazo zimekidhi vigezo hivyo kikamilifu.

### **6.10 Ushirikiano kati ya Sekta ya Umma na Binafsi**

58. Ushirikiano baina ya sekta ya umma na binafsi (PPP) ni miongoni mwa njia ya kutafuta fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Pamekuwepo mafanikio katika utekelezaji wa mfumo wa PPP hususan marekebisho ya sheria ya PPP ya mwaka 2014 na utekelezaji wa baadhi ya miradi kama vile mabasi yaendayo haraka (DART).

59. Ili kukuza utekelezaji wa miradi ya PPP, vipaumbele vitatolewa kwa miradi ambayo imefanyiwa upembuzi yakinifu kama vile: mradi wa tozo ya barabara wa Dar – Chalinze; uzalishaji wa dawa na vifaa tiba; na mtambo wa uzalishaji wa umeme wa gesi wa Kinyerezi III. Kila Wizara, Idara zinazojitegemea, Taasisi na Wakala za Serikali, Mashirika ya Umma, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatakiwa kukamilisha upembuzi yakinifu ili kuwezesha miradi hiyo kutekelezwa kupitia mfumo wa PPP. Katika kuanzisha miradi ya PPP na kujenga uwezo wa kitaasisi, Serikali itaendelea kutenga fedha kwenye Mfuko wa Uwezesaji wa PPP.

60. Kila Wizara, Idara zinazojitegemea, Taasisi na Wakala za Serikali, Mashirika ya Umma, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinazotarajia kushirikiana na sekta binafsi zinapaswa kufanya upembuzi yakinifu kwa kina kabla ya kuingia makubaliano ya kutekeleza miradi hiyo. Maafisa Masuuli wanapaswa:

- a) Kujenga mazingira bora ya kuvutia ushiriki wa sekta binafsi;

- b) Kujumuisha miradi ya PPP katika mipango na mikakati ya sekta zao; na
- c) Kubainisha miradi itakayovutia uwekezaji wa sekta binafsi na kuiwasilisha kituo cha PPP kwa ajili ya uchambuzi kulingana na sheria ya PPP. Kwa upande wa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, miradi ya PPP inapaswa kuwasilishwa Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa ajili ya uchambuzi na uidhinishwaji kabla ya kuwasilishwa katika kituo cha PPP.

61. Ofisi ya Waziri Mkuu itatakiwa kuanzisha na kuendesha kituo cha PPP na kuandaa na kusambaza vigezo na miongozo ya kuchambua mahitaji ya fedha za upembuzi yakinifu kupitia mfuko wa uwezeshaji wa PPP. Kadhalika, Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango itatoa utaratibu wa kuhakikisha kila Wizara, Idara zinazojitegemea, Taasisi na Wakala za Serikali, Mashirika ya Umma, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinajumuisha miradi ya PPP katika mipango na mikakati ya sekta zao.

## **7.0 MAELEKEZO MAHSUSI KWA SEKRETARIETI ZA MIKOA NA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA**

62. Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa wakati wa uandaaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2016/17 zitatakiwa kuzingatia yafuatayo:

- a) Kudumisha amani, utulivu na usalama katika maeneo yao ya utawala;
- b) Kuendesha mikutano ya kisheria (Mikutano ya vijiji, RCC, DCC na ujirani mwema);
- c) Kupitia na kuimarisha utekelezaji wa sera ya ugatuzi katika maeneo yao ya utawala kwa ajili ya kuboresha utoaji wa huduma kwakuwawezesha watu katika kada ya chini (vijiji na Kata);
- d) Kuandaa Mipango Mikakati ya mikoa na Serikali za Mitaa sambamba na Mpango wa Maendeleo ya mwaka 2016/17, maelekezo ya OR - TAMISEMI na Ilani ya Uchaguzi wa Chama Tawala wa mwaka 2015;
- e) Kuimarisha maendeleo endelevu ya matumizi ya ardhi kulingana na mipango ya vijiji na miji, upimaji wa ardhi, na kutenga maeneo madogo, ya kati na makubwa kwa ajili ya viwanja na maendeleo ya kilimo na ujenzi wa miundombinu ya maji, shule, huduma za afya, vituo vya mabasi, masoko na sehemu za mapumziko;
- f) Kuanzisha na kurasimisha utengaji wa maeneo kwa ajili ya kilimo, ufugaji, makazi, hifadhi ya wanyama na misitu, vyanzo vya maji na uwekezaji katika maeneo yote ya halmashauri ili kuzuia kutokea migogoro isiyo ya lazima na gharama za fidia;
- g) Kutekeleza mwongozo wa serikali mtandao katika Sekretarieti za mikoa na serikali za mitaa, kwa ajili ya kuboresha utoaji wa huduma. Hii ni pamoja na malipo kwa mtandao na juhudi za kuhuisha mifumo iliyopo kama vile I-Tax,

- LGRCIS, IFMS, PlanRep, LGMD, CDR, CFR na HCMIS ili kukuza ukusanyaji wa mapato, ufuatiliaji na tathmini na kutoa taarifa ya shughuli za maendeleo;
- h) Kuboresha usafi wa mazingira kwa kuimarisha uwezo wa kitaasisi katika usimamizi wa taka – maeneo ya kukusanyia, kusomba na mashimo ya taka, miundombinu ya taa za barabarani, vyoo vya jumuiya na mfumo wa maji taka;
  - i) Kuimarisha timu za afya za mikoa na serikali za mitaa ili kuhakikisha upatikanaji wa huduma za afya zilizo boreshwa katika halmashauri, mikoa na hospitali za rufaa pamoja na huduma maalum, kuimarisha ubora wa afya na huduma za lishe na kuongeza upatikanaji wa huduma za lishe katika ngazi ya jamii na vituo vya kutolea huduma;
  - j) Kuimarisha tathmini na ufuatiliaji katika ngazi zote ili kuhakikisha utekelezaji wa mipango na miradi;
  - k) Kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya halmashauri na kuhakikisha kuwa asilimia 60 ya mapato inatengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Mapato hayo ni lazima yatolewe taarifa kati Fomu namba 4 ya MTEF;
  - l) Kuendelea na ujenzi/ukarabati na kuzipatia vifaa ofisi na makazi ya Wakuu wa Mikoa na Wilaya, Maafisa Tawala wa Mikoa na Wilaya; Ofisi za Kata na Vijiji. Ujenzi uzingatie nyumba 149 za maafisa wa ngazi za juu wa serikali zinazoendelea kujengwa na TBA;
  - m) Kujenga, kurekebisha na kuimarisha miundombinu ya kijamii na kiuchumi hasa katika sekta ya elimu, maji, afya, kilimo, mifugo, uvuvi na barabara kwa kuzingatia ubora wa kitaifa;
  - n) Kuwasilisha MTEFs na miradi mipya Ofisi ya Rais -TAMISEMI kwa ajili ya kupitiwa na kubaini mapungufu;
  - o) Kutekeleza shughuli ambazo fedha zake zilivuka mwaka kwa kuzingatia kifungu cha 29(3) ya Sheria ya Bajeti No. 11 ya mwaka 2015 na Kanuni zake;
  - p) Kuanzisha na kuimarisha mifumo inayolinda haki za watoto ikiwa ni pamoja na wale walioko katika mazingira hatarishi, kuzingatia mambo ya jinsia, mazingira, UKIMWI, kuzuia rushwa; Malengo ya Maendeleo Endelevu, na kukusanya takwimu;
  - q) Kuanzisha na kuimarisha kamati za kijamii za usimamizi wa maji, kama vile COWSCO na kuhakikisha upatikanaji endelevu wa maji safi;
  - r) kuimarisha usimamizi wa huduma za ugani kimasoko katika kuhakikisha inaendana na sera ya ugatuzi, pamoja na kuongeza ushiriki wa sekta binafsi katika kilimo na maendeleo ya viwanda;
  - s) Kuwekeza katika vyanzo vya mapato ili kuhakikisha upatikanaji wa kudumu wa mapato. Kulinganana mchango wa mapato katika serikali za mitaa hasa kwa ushuru wa mazao, halmashauri zinatakiwa zitenge asilimia 60 kwa ajili ya miradi ya maendeleo ikijumuisha asilimia 20 kwa ajili ya kilimo, asilimia 15 kwa ajili ya mifugo, na asilimia 5 kwa ajili ya uvuvi;

- t) Kuboresha mazingira ya biashara kwa kuanzisha kituo kimoja kwa ajili ya kutolea vibali vya ujenzi, leseni za biashara, ukaguzi wa majengo yanayojengwa na utoaji wa hati za ardhi;
- u) Kuimarisha ukuzaji wa mazao ya kilimo na biashara na kuhakikisha usalama wa chakula;
- v) Kukuza SMEs, SACCOS, VICOBA na makundi mengine ya kijamii kwa ajili ya uzalishaji wa ajira; na
- w) Kuwezesha uendelezaji wa EPZA na SEZ kwa kukamilisha malipo ya fidia na ujenzi wa miundombinu.

## **8.0 UFUATILIAJI, TATHIMINI NA UTOAJI TAARIFA**

63. Ufuatiliaji na tathmini (M&E) una umuhimu mkubwa katika kutekeleza mpango na bajeti. Kwa kutambua hilo, serikali imejumuisha kazi za M&E katika majukumu ya wizara na idara za serikali, Sekretarieti za Mkoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa ikiwa ni pamoja na kuanzisha vitengo vya M&E chini ya idara za Sera na Mipango pamoja na kujengea uwezo eneo hilo. Mbali na jitihada hizo, kazi za M&E na utoaji wa taarifa za kiutendaji serikalini bado zinakabiliwa na changamoto nyingi zikiwemo:

- a) Kukosekana kwa mfumo jumuisi wa kuratibu ufuatiliaji na tathmini Serikalini;
- b) Uhaba wa watendaji kwenye vitengo vya M&E;
- c) Ukosefu wa taaluma na ujuzi mchanganyiko;
- d) Uhaba wa fedha kwenye ufuatiliaji na tathmini; na
- e) Vitengo vya M&E kutohusisha kazi za kufanya tathmini.

64. Katika kukabiliana na changamoto hizo, serikali itahakikisha kuwa inaimarisha uwezo wa kitaasisi ili kumudu vyema kazi za ufuatiliaji na kufanya tathmini. Afisa masuhuli wote wanaelekezwa kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya shughuli za M&E.

### **8.1 Utoaji wa Taarifa za Utendaji**

65. Kulingana na kifungu cha 55(4) cha sheria ya bajeti Na. 11 ya Mwaka 2015 na kanuni ya 30 (5), Maafisa Masuuli wote wanapaswa kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango kila robo mwaka taarifa za utekelezaji ndani ya siku 30 kila baada ya kumaliza robo mwaka.

66. Vile vile, kuhusu taarifa ya utekelezaji ya mwaka, Maafisa Masuuli wanapaswa kutayarisha taarifa ya kina inayoonesha mafanikio yaliyopatikana katika kipindi husika. Mafanikio hayo ni lazima yawiane na viashiria vya utendaji na malengo ya mwaka. Aidha, taarifa hiyo ni lazima ioneshe mafanikio na changamoto kwenye

maeneo maususi kama vile: makusanyo ya mapato; matumizi; na hali ilivyo kuhusu rasilimali watu. Vile vile, taarifa hiyo ya mwaka inatakiwa kuandaliwa na kuwasilishwa Wizara ya Fedha na Mipango si zaidi ya tarehe 15 Oktoba, baada ya mwisho wa mwaka wa fedha. Taarifa hizo za robo mwaka na ile ya mwaka ya utekelezaji ziwasilishwe kwenye nakala ngumu na nakala laini Wizara ya Fedha na Mipango, PO-PSMGG, PMO, PO-RALG na OTR.

## **8.2 Mwisho**

67. Serikali inatarajia kuwa utekelezaji wa vipaumbele vilivyoainishwa kwenye Mwongozo wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2016/17 utachochea dhamira ya maendeleo katika Wizara, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi na Mashirika ya Umma kwa kuzingatia maelekezo yaliyotolewa kwenye Mwongozo huu. Hivyo, Maafisa Masuuli wanalazimika kuzingatia Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015 pamoja na kanuni zake. Aidha, Maafisa Masuuli wanapaswa kutenga fedha kwa lengo la kuboresha utekelezaji wa maeneo muhimu yaliyoainishwa kwenye mpango wa maendeleo kwa mwaka 2016/17 unaolenga katika maendeleo ya viwanda na maendeleo ya watu. Vile vile, Mpango na Bajeti utazingatia malengo yaliyomo kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 pamoja na mikakati mingine inayolenga kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025. Maafisa masuulii wanaelekezwa kufuatilia utekelezaji wa Mpango na Bajeti ili kupata thamani ya fedha na kuhimiza uwajibikaji.

Table 1: Tentative Likely Outturn for 2015/16 and Estimated Baseline for 2016/17

TRA MAINLAND	Budget 2015/16	December YTD 2015			Estimates January - June, 2016	2015/16 Likely Outturn	Perf. Likely Outturn	Shs.Million	
		Estimate YTD	ActualYTD	Perf. YTD				2016/17	Baseline Growth to 2016/17
								Baseline	
<b>GDPmp</b>	<b>94,804,705</b>	<b>94,804,705</b>	<b>94,804,705</b>		<b>94,804,705</b>	<b>94,804,705</b>		<b>106,888,643</b>	
<b>Revenue/GDP ratio</b>	<b>13.0%</b>	<b>6.4%</b>	<b>6.4%</b>		<b>6.6%</b>	<b>13.0%</b>		<b>13.2%</b>	
<b>TOTAL TRA</b>	<b>12,362,958.5</b>	<b>6,095,438.2</b>	<b>6,040,388.6</b>	<b>99.1%</b>	<b>6,267,519.8</b>	<b>12,307,908.4</b>	<b>99.6%</b>	<b>14,139,015.9</b>	<b>14.9%</b>
<b>Add Treasury voucher</b>	<b>32,413.6</b>	<b>16,206.8</b>	<b>11,927.7</b>	<b>73.6%</b>	<b>16,206.8</b>	<b>28,134.5</b>	<b>86.8%</b>	<b>32,413.6</b>	<b>15.2%</b>
<b>Net Collections</b>	<b>12,330,544.9</b>	<b>6,079,231.4</b>	<b>6,028,460.9</b>	<b>99.2%</b>	<b>6,251,313.0</b>	<b>12,279,773.9</b>	<b>99.6%</b>	<b>14,106,602.4</b>	<b>14.9%</b>
<b>Less Tax Refunds</b>	<b>857,293.8</b>	<b>431,550.3</b>	<b>345,483.5</b>	<b>80.1%</b>	<b>425,743.5</b>	<b>771,227.0</b>	<b>90.0%</b>	<b>925,901.7</b>	<b>20.1%</b>
<b>GRAND TOTAL</b>	<b>13,187,838.7</b>	<b>6,510,781.7</b>	<b>6,373,944.4</b>	<b>97.9%</b>	<b>6,677,056.5</b>	<b>13,051,000.9</b>	<b>99.0%</b>	<b>15,032,504.1</b>	<b>15.2%</b>
<b>DIRECT TAXES</b>	<b>4,557,288.7</b>	<b>2,228,361.9</b>	<b>2,318,656.4</b>	<b>104.1%</b>	<b>2,328,926.8</b>	<b>4,647,583.2</b>	<b>102.0%</b>	<b>5,298,686.4</b>	<b>14.0%</b>
P.A.Y.E.	2,045,493.3	1,004,732.9	1,090,270.0	108.5%	1,040,760.4	2,131,030.4	104.2%	2,417,924.1	13.5%
B. Skills & Dev.Levy	249,460.7	123,258.3	124,129.8	100.7%	126,202.4	250,332.3	100.3%	284,033.7	13.5%
Individuals	145,814.7	69,518.7	58,475.3	84.1%	76,296.0	134,771.3	92.4%	154,410.2	14.6%
Corporate Taxes	1,279,696.5	622,969.5	663,687.6	106.5%	656,727.0	1,320,414.6	103.2%	1,515,821.3	14.8%
Withholding taxes	715,241.7	349,778.8	320,345.0	91.6%	365,462.9	685,807.9	95.9%	784,820.2	14.4%
Rental Tax	76,547.2	36,633.1	38,754.8	105.8%	39,914.2	78,669.0	102.8%	89,410.8	13.7%
Gaming Tax	22,349.6	10,655.4	7,969.0	74.8%	11,694.2	19,663.2	88.0%	22,343.6	13.6%
All Other direct taxes	22,685.0	10,815.3	15,024.8	138.9%	11,869.7	26,894.5	118.6%	29,922.5	11.3%
Less Income Tax Refunds	8,584.3	4,292.2	4,123.3	96.1%	4,292.2	8,415.4	98.0%	9,488.1	12.7%
<b>INDIRECT TAXES</b>	<b>8,630,550.0</b>	<b>4,282,419.8</b>	<b>4,055,288.0</b>	<b>94.7%</b>	<b>4,348,129.8</b>	<b>8,403,417.8</b>	<b>97.4%</b>	<b>9,733,817.7</b>	<b>15.8%</b>
<b>CONSUMPTION TAXES</b>	<b>2,981,274.0</b>	<b>1,490,993.3</b>	<b>1,332,690.1</b>	<b>89.4%</b>	<b>1,490,280.3</b>	<b>2,822,970.3</b>	<b>94.7%</b>	<b>3,377,819.4</b>	<b>19.7%</b>

TRA MAINLAND	Budget 2015/16	December YTD 2015			Estimates January - June, 2016	2015/16 Likely Outturn	Perf. Likely Outturn	2016/17	Baseline Growth to 2016/17
		Estimate YTD	ActualYTD	Perf. YTD				Baseline	
<b>Excises (Domestic)</b>	<b>995,992.6</b>	<b>489,569.1</b>	<b>451,969.0</b>	<b>92.3%</b>	<b>506,423.5</b>	<b>958,392.5</b>	<b>96.2%</b>	<b>1,094,053.3</b>	<b>14.2%</b>
Beer	242,412.2	117,957.1	117,892.0	99.9%	124,455.0	242,347.0	100.0%	274,855.5	13.4%
Cigarettes	164,880.4	84,597.1	71,538.2	84.6%	80,283.3	151,821.5	92.1%	172,154.3	13.4%
Soft Drinks	47,391.8	23,792.0	19,898.9	83.6%	23,599.8	43,498.7	91.8%	49,383.8	13.5%
Bottled Water	19,938.6	10,145.6	6,947.0	68.5%	9,793.0	16,740.0	84.0%	19,195.0	14.7%
Mobile Phone	307,452.4	150,477.6	127,047.8	84.4%	156,974.8	284,022.6	92.4%	331,649.5	16.8%
Spirits	145,139.9	68,180.6	57,431.4	84.2%	76,959.3	134,390.7	92.6%	152,580.2	13.5%
All Other Excises (Domestic)	68,777.3	34,419.1	51,213.8	148.8%	34,358.2	85,572.0	124.4%	94,235.0	10.1%
<b>Aggregate VAT</b>	<b>1,985,281.4</b>	<b>1,001,424.2</b>	<b>880,721.0</b>	<b>87.9%</b>	<b>983,856.8</b>	<b>1,864,577.8</b>	<b>93.9%</b>	<b>2,283,766.10</b>	<b>22.5%</b>
<b>VAT Domestic Products</b>	<b>714,623.7</b>	<b>355,921.4</b>	<b>233,624.3</b>	<b>65.6%</b>	<b>358,703.0</b>	<b>592,327.3</b>	<b>82.9%</b>	<b>737,667.6</b>	<b>24.5%</b>
Beer	235,572.1	117,890.9	76,467.6	64.9%	117,681.2	194,148.7	82.4%	244,453.3	25.9%
Cigarettes	88,501.6	44,280.0	28,832.8	65.1%	44,221.5	73,054.4	82.5%	94,469.0	29.3%
Soft Drinks	92,199.2	35,491.5	21,942.9	61.8%	56,707.6	78,650.6	85.3%	101,705.6	29.3%
Cement	40,239.0	19,997.1	12,120.1	60.6%	20,241.9	32,362.0	80.4%	40,012.9	23.6%
Sugar	66,011.2	41,110.3	19,410.2	47.2%	24,901.0	44,311.1	67.1%	54,787.0	23.6%
Others	192,100.6	97,151.6	74,850.8	77.0%	94,949.8	169,800.6	88.4%	202,239.8	19.1%
<b>VAT Domestic Services</b>	<b>1,270,657.8</b>	<b>645,502.8</b>	<b>647,096.7</b>	<b>100.2%</b>	<b>625,153.8</b>	<b>1,272,250.5</b>	<b>100.1%</b>	<b>1,546,099</b>	<b>21.5%</b>
Electricity	243,424.4	121,899.3	55,039.5	45.2%	121,525.2	176,564.7	72.5%	220,310.3	24.8%
Telephones	370,737.7	181,547.1	107,833.3	59.4%	189,190.6	297,023.9	80.1%	370,614.5	24.8%
Retailers	25,176.1	13,317.6	11,717.0	88.0%	11,858.4	23,575.4	93.6%	32,809.3	39.2%
Wholesalers	33,974.9	18,030.3	14,125.5	78.3%	15,944.6	30,070.2	88.5%	36,156.0	20.2%
Transport	56,151.4	28,989.3	21,095.8	72.8%	27,162.1	48,258.0	85.9%	56,929.9	18.0%
Hotel Services	79,968.7	40,549.2	25,678.5	63.3%	39,419.5	65,098.0	81.4%	76,943.8	18.2%
Other	461,224.5	241,170.0	411,607.0	170.7%	220,053.3	631,660.3	137.0%	752,334.8	19.1%
Less VAT Refunds	489,224.9	258,879.9	277,836.8	107.3%	244,612.5	522,449.3	106.8%	589,041.4	12.7%
Add DRD Treasury Vouchers	9,778.6	4,889.3	608.9	12.5%	4,889.3	5,498.2	56.2%	9,778.6	77.9%
Add VAT Tax refunds returned	-	-	50,000.0		-	50,000.0		-	-100.0%

TRA MAINLAND	Budget 2015/16	December YTD 2015			Estimates January - June, 2016	2015/16 Likely Outturn	Perf. Likely Outturn	2016/17	Baseline Growth to 2016/17
		Estimate YTD	ActualYTD	Perf. YTD				Baseline	
Less: Transfer to ZRB	38,000.0	19,000.0	5,577.9	29.4%	19,000.0	24,577.9	64.7%	27,710.6	12.7%
Less: VETA	67,720.2	33,860.1	-	0.0%	33,860.1	33,860.1	50.0%	38,176.0	12.7%
Less: Bed night levy	3,331.5	1,665.8	-	0.0%	1,665.8	1,665.8	50.0%	1,878.1	12.7%
Less: MV D/licence	9,223.7	4,611.9	4,609.8	100.0%	4,611.9	9,221.7	100.0%	10,397.1	12.7%
Less: Departure charges	62,142.3	33,974.5	-	0.0%	28,167.8	28,167.8	45.3%	31,758.1	12.7%
Less: MV D/licence								-	
<b>OTHER Domestic Taxes &amp; Charges</b>	<b>344,046.7</b>	<b>184,517.8</b>	<b>146,243.0</b>	<b>79.3%</b>	<b>159,529.0</b>	<b>305,772.0</b>	<b>88.9%</b>	<b>348,244.1</b>	<b>13.9%</b>
Departure charges	62,142.3	33,974.5	36,954.9	108.8%	28,167.8	65,122.7	104.8%	72,454.8	11.3%
Motor Vehicle Taxes	269,241.8	143,944.7	102,078.3	70.9%	125,297.1	227,375.4	84.5%	260,719.5	14.7%
Stamp Duty	12,662.7	6,598.6	7,209.8	109.3%	6,064.1	13,274.0	104.8%	15,069.9	13.5%
<b>TOTAL CED</b>	<b>5,148,797.4</b>	<b>2,542,960.3</b>	<b>2,484,338.0</b>	<b>97.7%</b>	<b>2,661,739.9</b>	<b>5,189,795.2</b>	<b>100.8%</b>	<b>5,812,936.8</b>	<b>12.0%</b>
<b>Add CED Treasury voucher</b>	<b>22,635.0</b>	<b>11,317.5</b>	<b>11,318.8</b>	<b>100.0%</b>	<b>11,317.5</b>	<b>22,636.3</b>	<b>100.0%</b>	<b>22,635.0</b>	<b>0.0%</b>
<b>CED Net Collections</b>	<b>5,126,162.4</b>	<b>2,531,642.8</b>	<b>2,473,019.1</b>	<b>97.7%</b>	<b>2,650,422.4</b>	<b>5,167,158.9</b>	<b>100.8%</b>	<b>5,790,301.8</b>	<b>12.1%</b>
<b>Less CED Tax Refunds</b>	<b>179,066.8</b>	<b>75,265.9</b>	<b>103,335.7</b>	<b>137.3%</b>	<b>47,898.1</b>	<b>107,516.5</b>	<b>60.0%</b>	<b>217,452.5</b>	<b>102.3%</b>
<b>INTERNATIONAL TRADE TAXES</b>	<b>5,305,229.2</b>	<b>2,606,908.7</b>	<b>2,576,354.9</b>	<b>98.8%</b>	<b>2,698,320.5</b>	<b>5,274,675.4</b>	<b>99.4%</b>	<b>6,007,754.3</b>	<b>13.9%</b>
<b>Import Duties</b>	<b>1,233,922.2</b>	<b>606,330.5</b>	<b>616,573.5</b>	<b>101.7%</b>	<b>627,591.7</b>	<b>1,244,165.1</b>	<b>100.8%</b>	<b>1,359,523.1</b>	<b>9.3%</b>
Non-Petroleum Imports	863,989.7	424,551.3	409,017.8	96.3%	439,438.3	848,456.2	98.2%	932,274.6	9.9%
Export Duty Levy	84,890.5	41,713.9	28,664.4	68.7%	43,176.6	71,841.0	84.6%	76,416.4	6.4%
Processing Fee-REA	15,975.5	7,850.1	10,183.1	129.7%	8,125.4	18,308.5	114.6%	20,125.0	9.9%
Railway Development Levy	125,761.8	61,797.4	76,126.1	123.2%	63,964.4	140,090.4	111.4%	149,027.4	6.4%
Processing Fee-dry cargo-TRA	53,304.7	26,193.1	29,991.3	114.5%	27,111.6	57,102.9	107.1%	62,561.9	9.6%
Water supply and sanitation	90,000.0	44,224.6	62,590.7	141.5%	45,775.4	108,366.1	120.4%	119,117.9	9.9%
<b>Excise Duties</b>	<b>960,507.5</b>	<b>471,978.7</b>	<b>637,007.8</b>	<b>135.0%</b>	<b>488,528.8</b>	<b>1,125,536.5</b>	<b>117.2%</b>	<b>1,231,739.2</b>	<b>9.4%</b>
Non-Petroleum Imports	235,167.9	115,557.9	264,082.4	228.5%	119,610.0	383,692.4	163.2%	416,291.5	8.5%
Petroleum imports	725,339.6	356,420.8	372,925.4	104.6%	368,918.8	741,844.1	102.3%	815,447.8	9.9%
<b>VAT on Imports</b>	<b>2,042,242.8</b>	<b>1,003,526.9</b>	<b>817,405.4</b>	<b>81.5%</b>	<b>1,038,715.8</b>	<b>1,856,121.2</b>	<b>90.9%</b>	<b>2,263,851.5</b>	<b>22.0%</b>
Non-Petroleum Imports	2,042,242.8	1,003,526.9	817,405.4	81.5%	1,038,715.8	1,856,121.2	90.9%	2,263,851.5	22.0%

TRA MAINLAND	Budget 2015/16	December YTD 2015			Estimates January - June, 2016	2015/16 Likely Outturn	Perf. Likely Outturn	2016/17	Baseline Growth to 2016/17
		Estimate YTD	ActualYTD	Perf. YTD				Baseline	
Petroleum Levy Fee- REA	238,021.9	116,960.4	134,019.3	114.6%	121,061.6	255,080.9	107.2%	280,389.3	9.9%
Fuel Levy	810,264.0	398,151.4	362,285.9	91.0%	412,112.6	774,398.5	95.6%	851,232.1	9.9%
Non-Tax Revenue	20,270.9	9,960.8	9,063.0	91.0%	10,310.1	19,373.1	95.6%	21,019.0	8.5%
Less Customs & Excise Refunds	38,726.4	19,363.2	19,363.2	100.0%	19,363.2	38,726.4	100.0%	43,662.5	12.7%
Less VAT-Mining	57,069.8	14,267.5	40,255.2	282.1%	28,534.9	68,790.1	120.5%	77,558.2	12.7%
Less: Transfer to Customs proc. Fees- dry cargo TRA	58,874.2	29,437.1	43,717.4	148.5%	29,437.1	73,154.5	124.3%	82,478.8	12.7%
Less: Transfer ProcessingFee-REA	1,241.9	620.9	-	0.0%	620.9	620.9	50.0%	700.1	12.7%
Less: Transfer Export Duty-Cashewnut Board	23,154.4	11,577.2	-	0.0%	11,577.2	11,577.2	50.0%	13,052.9	12.7%
CED Treasury Vouchers	22,635.0	11,317.5	11,318.8	100.0%	11,317.5	22,636.3	100.0%	22,635.0	0.0%